# JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT TEST

PIONEER MARK SERIES

## GREDI YA NANE - 2025

## KISWAHILI

Jina: ____________________________________________

Shule: ____________________ Nambari ya usajili. ________Tarehe:________

### VIWANGO VYA KUZINGATIA KATIKA KUTATHIMINI.

| KUZIDI MATARAJIO | KUFIKIA MATARAJIO | KUKARIBIA MATARAJIO | MBALI NA MATARAJIO | JUMLA (ALAMA %) |
|---|---|---|---|---|
| 35-50 | 26-34 | 15-25 | 0-14 | |

### SEHEMU YA A: UFAHAMU

**Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Ni jambo lisilopingika kuwa elimu ni ufunguo wa maisha. Aidha elimu ni nguze imara ya kuegemea maishani hata hivyo, yafaa ifahamike kuwa elimu itamfaidi mmiliki wayo yule ambaye ataitumia kwa ufasaha. La muhimu zaidi yule ambaye ataitumia kwa nidhamu, hekima na heshima

Haijalishi iwapo mahuluki ameyasoma matopa ya vitabu. Haijalishi amefika kiwango kipi au anazo shahada zipi? Iwapo hana adabu, heshima, nidhamu na uajibikaji elimu yako haijakamilika. Elimu hiyo yote si lolote si chochote. Elimu yake itakuwa kama pambo wala si lebasi. Pambo haliwezi kusitiri mtu. Hiyo ni kazi ya nguo.

Ni fedheha na izara kuwaona baadhi ya insi wakichachawiza kuwa wameelimika ilhali wanazo fuska. Heshima kwao ni mwiko. Adabu kwao ni neno geni. Ukweli ni kuwa elimu hiyo yao haina faida kwa walimwengu. Mwalimu wangu wa zamani alinieleza kuwa kumiliki elimu ya aina hiyo ni sawa na kufunga tai huku mtu akiwa uchi wa mnyama.

Ni jambo aula mtu kuonyesha elimu yake kwa vitendo. Vitendo vya yeyote aliye na elimu vinafaa view na mwelekeo na vya kutamanika. Vionyeshe ustaarabu wala si ushenzi.

Aidha ifahamike kuwa elimu si ya vitabu tu. La hasha! Ipo pia elimu dunia. Sharti elimu yetu ituwezeshe kutafakari ya dunia

**MASWALI**

1. Ni jambo lipi lisilopingika kuhusu elimu (al 1)

   ..........................................................................................................

2. Ni nani anayefaidika sana na elimu aliyo nayo(al 1) ..........................................

3. Elimu bora ni ipi?

   A) Ya chuo kikuu B) Yenye uajibikaji C) Ya nyumbani D. Inayoheshimiwa

4. Mtu hutajika ameelimika ikiwa (al 1)

   A) Amesoma matopa ya vitabu B) Ana msururu wa shahada

   C) Ana fuska D) Ana ustaarabu

5. Ni kweli kusema (al 1)

   A) Yeyote aliye na elimu ni mstaarabu B) Asiye na elimu ni mshenzi

   C) Matendo mema hupita elimu D) Elimu si ufunguo wa maisha

6. Kisawe cha neno lebasi ni________________________________________(1 al)

7. Ni jambo aula.........." Inamaanisha(AL 1)

..............................................................................................................................

8. Mwandishi ametaja aina ngapi za elimu________________________________(AL 1)

9. Lengo kuu la elimu ni lipi? (al 1)

A) Kuwajibika
B) Kumtajirisha mmiliki
C) Kusifika kwa mmiliki
D) Kuelewa kufanya kazi mbalimbali

10. Taja mada mwafaka ya kifungu hiki

..............................................................................................................................

**Soma kifungu kifuatacho kish ujibu maswali 11-15**

Mwongo mmoja baadaye ukeketaji ukatoweka kwenye msamiata wa jamii yake. Wakeketaji hao wakawa wamejiona kama waliovuliwa nguo.

Mabadiliko yakapatikana kwa ujasiri wa Maria ambaye kujitlea kwake mhanga kuliko maisha ya wengi uchochole umemgandama, lakini ufanisi umempa adhama.

11. Mwongo mmoja ni ________________________________________(al 2)

12. Jamii ya akina maria ilikuwa ikiwafanyia wanawake dhuluma gani? (al 1)

..............................................................................................................................

13. Ujasiri wa maria ulileta mabadiliko yapi? (al 1)

..............................................................................................................................

14. *Hata kama Maria amefanikiwa katika azimio lake, ni jambo lipi linalofanya jamii imwonee huruma? (al 1)*

..............................................................................................................................

15. Neno "adhama" lina maana gani kwa mujibu wa taarifa hii? (al 1)

A) Woga B) Ukubwa C) Dharau D) Pongezi

**SEHEMU YA B: MATUMIZI YA LUGHA. (al 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu nafaji ukitumia maneno uliyopewa hapo chini.**

Sote tuliajabia bidhaa mbalimbali alizounda katika____16____ ile yake ya uhunzi. Alikuwa amefua______17____. Hakika______18____ wake ulibainika ____19____ kutokana na uzuri wa vyombo hivyo. Isitoshe, kipato anachopata kutokana na mauzo ya bidhaa zenyewe kilituacha____20____ kwa mshangao. Hapa ndipo nilipong'amua kuwa si lazima ning'ang'anie kazi za ofisini kama wafanyavyo vijulanga wengine.

16. A) Duka B) Karakana C) Kiwanda D) Zahanati

17. A) Mikufu,miundu na visu
B)mashoka, pete,nyungu
C) Meza, masofa na madawati
D) Majembe, masufuria, sanduku

18. A) Ukali B) Bidii C) Umahiri D) Nidhamu

19. A) Dhahiri shahiri
B) Salama salimini
C) Bure bilashi
D) Raha mustarehe

20. A) Mikono juu B) Tumefumba macho C) Pumzi juujuu D) Vinywa wazi

21. Tambua kisha upigie mstari viwakilishi vya nafsi katika sentensi zifuatazo. (al 2)

A) nyinyi hupiga deki madarasa yenu lini?

B) Sisi tulizoa taka na kuzipeleka kwenye jaa

22. Jaza nafasi zilizoachwa kwa kutumia viwalikilishi vya pekee vifaavyo. Chagua jibu kutoka kwenye mabano. (al 2)

A) ____________________umeliwa (sote, yote,wote)

B) ____________________ lilifunga kabla hatujaingia. (lenyewe, yenyewe, chenyewe)

23. Badilisha sentensi zifuatazo kutoka wakati uliopo hadi hali ya mazoea. (al 2)

A) Mimi ninalima sasa

..........................................................................................

B) Wewe unakula

..........................................................................................

24. Badilisha sentensi zifuatazo kutoka hali ya mazoea hadi hali timilifu. (al 2)

A) Jua huchomoza.

..........................................................................................

B) Upepo huzalisha kawi.

..........................................................................................

25. Badilisha sentensi ulizopewa Katika jedwali kuonyesha wakati unaolengwa. (al 2)

| Wakati uliopita hali timilifu | Wakati ujao hali timilifu |
|---|---|
| A. Daktari alikuwa amewahudumia wangonjwa wote | |
| B. | Mvuvi atakuwa amefika sokoni gari litakapowasili |

## FASIHI

26. Soma sehemu ifuatayo ya kifungu, kisha ujibu maswali. (al 4)

Maisha ya gera yalizidi kuwa magumu kila siku. Nilijikaza katika masomo yangu huku musambale akinihimiza kila wakati kutia bidi. Maisha ya upweke yaliendelea kunisonga pia. Ingawa tuliishi katika nyumba moja bila kupendana wala kuwa na ushirikiano wowote. Tulikosa utangamano waliokuwa nao watu walioishi katika nyumba moja. Ungedhani nyumba hiyo kulikaa fisi na mbuzi. Aibu iliyoje!

a) Eleza maudhui yanayojitokeza katika kifungu ulichosoma. (al 2)

..........................................................................................

..........................................................................................

b) Taja angalau wahusika wawili waliotajwa katika kifungu (al 1)

i. ........................................ ii. ........................................

c) Taja mandhari ya kimahali katika kifungu (al 1)

..........................................................................................

27. Eleza vipengele viwili vinavyozingatiwa katika uwasilishaji wa mighani (al 2)

i. ........................................ ii. ........................................

28. Taja sifa mbili za mighani (al 2)

..........................................................................................

..........................................................................................

29. Eleza maana ya tamthilia. (al 1)

..........................................................................................

30. Taja sifa mbili za visasili. (al 1)

..........................................................................................

..........................................................................................

## INSHA (AL 10)

Mwandikie rafiki yako barua ili kumwalika katika dhifa ya kusherehekea siku ya kuzaliwa kwako.

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................

................................................................................